**[R2251]**

## "BASI NINYI SALINI HIVI."

***MATHAYO. 6:5-15***

"Usali mbele za Baba yako aliye sirini."

"MAOMBI ni shauku ya dhati ya nafsi, inayotamkwa au isiyoelezeka ," asema mtunzi wa mashairi: na yuasema ukweli kwa sababu Maandiko yanatufahamisha kwamba Mungu "ni mtambuaji wa mawazo na makusudi ya moyo;" na pia kwamba kwa watakatifu roho au nia inakubaliwa na Bwana tukimkaribia wakati wa shida,wakati hatuna lugha yo yote ya kutumia kwa kuvalisha hisia na hamu zetu,-tunapomjia kwa roho inayougua ambayo hatuwezi kutamka kwa maneno. (***Warumi. 8:26***) Hata hivyo kwa maneno na mfano Bwana wetu alitushauri kwamba maombi yetu yafaa yatamkwe,yaandaliwe na ikiwezekana,yasiachiliwe hisia zisizoweza kufungamana na mgumio. Ni kwa harakati hii ambapo aliyatoa maagizo yanayotumika sasa alipokuwa akijibu ombi la mitume, ‘’Bwana tufundishe sisi kusali."—***Luka 11:1***

Ijapo sheria nyingine zinapaswa kutawala maombi yote kwa jumla,njia zote za kumwomba Mungu kama vile,kumkaribia kwa unyenyekevu na unyofu wa moyo na heshima na katika jina la Yesu ,lakini hali zaweza kutawala wakati mwingine:—

(1) Maombi ya mwenye dhambi,mgeni na asiye mwenyeji kwa Mungu yanafaa kuwa tofauti na maombi ya *mtoto* wa Mungu ambaye amepata msamaha wa dhambi na kupata upatanisho kwa njia takatifu zilizoteuliwa.Kwa mfano,maombi ya mtoza ushuru,yaliyoidhinishwa na Bwana,hayakutaja Yehova kama ‘’Baba’’ lakini kama Mungu- ‘’Mungu nirehemu mwenye dhambi.’’ Kwa njia nyingine,wale wanaokuja katika uhusiano na Mungu kupitia sheria ya agano la Kristo wana fursa sio ya kumtambua Mungu pekee kama Muumbaji na Mtawala,lakini pia kama ‘’Baba wa Mbinguni,’’ na wanamtaja kama Baba.

(2) Miongoni mwa wale wanaomkaribia Mungu katika maombi kama watoto wake,mazingira na hali tofauti yawezakuwa na fani kulingana na namna ya kuabudu:wakati mwingine wanaweza kuenda kando vile inavyotakikana na kupata kushiriki na Baba mahali pa siri,-mahali ambapo jicho halioni na sikio la kidunia halitasikia.Mfano wa Bwana wetu unafaa uwe kielelezo cha fursa hii:Twakumbuka vile imeandikwa kumhusu kwamba kila mara alienda mbali na wanafunzi wake na kuomba akiwa peke yake,na jinsi kwa wakati mwingine aliomba usiku kucha akiomba peke yake.

(3) Maombi kwa wakati mwingine yaweza kutolewa kwa njia mwafaka na inayofaa mbele ya waumini wapendwa kwa sauti,kama maombi ya wengi ambayo wote wana hamu ya kushiriki.Ufafanuzi wa jambo hili laweza kupatikana kutoka kwa mfano wa Bwana wetu:Kwa mfano,maombi yake yalirekodiwa katika *Yohana 11:41,42;17;Mathayo 11:25,26;Luka 10:21;11:1.*Maombi haya hayangerekodiwa ikiwa hayakusikika na mitume:na hata sababu ya kutamkwa kwayo mbele yao ilikuwa ni kwa ajili yao na kuwabariki,na pia kwa waumini na baraka zao wote walioamini tangia wakati ule.Maombi ya Musa na Sulemani,Daudi na Yeremia,Ezekieli na Danieli yamerekodiwa pia,kwa hiyo yalifanywa hadharani,hasa mbele za watu wa Bwana.Rekodi kuhusu Kanisa la awali inaonyesha kwamba walikutanika pamoja kama familia moja na kwamba maombi yao na nyimbo zao pamoja na maombi kwa jumla yalikuwa sawa kwa ajili ya watu wote waliokuwako pale.Jambo hilo limedokezwa katika maelezo yaliyoko katika *Matendo 1:14* ambayo yanasema, ‘’Hawa wote walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja katika kusali,pamoja na wanawake,na Mariamu mama yake Yesu,na ndugu zake.’’ Tena,maneno ya mojawapo ya maombi yao yamenukuliwa katika *Matendo 1:24*; ombi hili dhahiri lilitamkwa

kwa sauti na kwa pamoja.Tena katika *1 Wakorintho 14:16* Mtume anaonyesha shukrani ya kusanyiko ilitolewa na inafaa itolewe mbele ya Bwana siyo tu kwa sauti pekee lakini katika lugha inayosikika na kueleweka na waumini ili kwamba wote waweze kuitikia kwa kusema ‘’Amina’’ kwa maombi ya shukrani na dua.

(4) Wakati mwingine si vizuri kumshukuru Mungu mbele ya kusanyiko mchanganyiko - ya waumini na wasioamini.Ufafanuzi wa jambo hilo linapatikana katika mwenendo wa Bwana mwenyewe.Maombi yake wakati wa ubatizo wake katika Mto Yordani yalishuhudiwa na umati.(*Luka 3:21*).Tena Bwana wetu aliomba hadharani akasikika na umati uliochanganyikana,kwa kaburi la Lazaro.Tena mwisho wa huduma ya Bwana wetu,wakati aliomba , ‘’Baba,niokoe kwa wakati huu,’’ ‘’Baba,litukuzwe jina lako,’’ umati uliozingira walisikia na kwa namna nyingine walijua maombi hayo kama vile ilivyoonyeshwa na maelezo ya *Yohana 12:29*.Tena,maombi ya mwisho ya Bwana wetu akiwa msalabani,yalitamkwa kwa sauti na yakasikika na hata maadui wake-*Mathayo 27:46,50*.

Tumeeleza kwa kina thibitisho kwa mada hii kwa sababu watu wengine wa Mungu wamefanya kosa kupitia somo hili ambalo tunaenda kuangalia,kudhani kwamba ni kosa,au ni dhambi kuomba na watu au mbele ya wengine,yaani mbele ya Kanisa au ulimwengu;wanaweka mkazo kwa maneno ya Bwana wetu aliyosema, ‘’ingia katika chumba cha ndani,n.k,’’ kuliko yale aliyokusudia Bwana wetu,kama vile tulivyoonyesha kutoka kwa mwenendo wake,ambao pia ndio ufafanuzi wa nguvu ya mafundisho yake, -kwa sababu ‘’Yeye hakutenda dhambi,wala hila haikuonekana kinywani mwake.’’ Hata hivyo ,tunasema kwamba hatuna huruma yo yote na vitendo ambavyo vimekuwa sawa kwa Wakristo wengi ,kama vile kuwahubiria wenye dhambi na kuwakemea katika maombi ya hadharani yanayotolewa kwa Mungu.Kwamba tabia hii ya kawaida inatambulika na wengine,inaelezwa na maelezo yafuatayo ambayo yalionekana katika jarida la kidunia la Bostoni,kwa maoni mazuri juu ya mahubiri ya mhudumu maarufu katika jiji hilo.Yalisema: ‘’Maombi yake kwa kawaida yalikubaliwa kama mojawapo ya maombi mazuri sana yaliyotolewa kwa hadhira ya Bostoni.’’ Kuna sababu za kipekee za kufanya tuamini kwamba maombi mengi yanayotolewa yanafanywa kwa makusanyiko ambao wanasikia kuliko kwa Mwenyezi.Huu ni upotoshaji wa fursa ya ajabu ya maombi ambayo watoto wa Mungu wamepewa,na pia inaendana na unafiki wa siku ya Bwana ambao aliwaonya wanafunzi kuhusu unafiki huo,akisema kwamba wale ambao wanasali ni wanafiki na ujira wao unasikika na watu,kwa sababu huo ndio ujira wanatafuta.

Hadi leo msafiri katika Mashariki ataona na kuyasikia maombi toka kila upande.Maombi mengine yanawezakuwa matokeo ya nguvu na dhamiri iliyokosa mwelekeo,na mengi bila shaka kama ilivyonenwa na Bwana wetu,ni matokeo ya kiburi cha kiroho na tamaa ya kudhaniwa kuwa wachamungu.Msafiri wa Mashariki aliandika yafuatayo: ‘’Niliamshwa asubuhi na mapema na sauti ya maombi ambayo yalitarajiwa kusikilizwa na watu ikiwa Mungu alipaswa kuyasikia ama kutosikia,yalikuwa marefu na sauti ya juu na kupaza sauti kila mara ambayo inaamsha yule ambaye amelala fofofo-alikuwa mkalimani,ambaye baada ya maamkuzi ya asubuhi,aliongeza, ‘’Je! Ulinisikia nikiomba asubuhi hii, bwana wangu?’’ Ndiyo nilisikia, nikamjibu.Baadaye akaniambia kuhusu juhudi na bidii yake katika maombi.’’Mapokeo ya Wakristo yanatofautiana,na katika pande zote tunapata uthibitisho wa roho kama hiyo-matarajio ya kudhaniwa kuwa mchamungu,jitihada ya kutoa hisia kwa wanaume na wanawake,badala ya kufanya ushirika na Baba wa Mbinguni.Unafiki wa namna hiyo hauwezi kuruhusiwa na wale wote wanaotafuta na kufurahia ushirika na Baba na Bwana wetu Yesu Kristo.

## JE! TWAPASWA KUOMBA KWA NANI?

Agizo la Bwana wetu ni kwamba,''Ombeni kwa Baba yangu,'' ''Salini hivi,Baba yangu uliye juu mbinguni.''Lakini agizo hili lafaa kuwekwa pamoja na agizo hili, ''lo lote mwombalo Baba kwa jina langu awapeni.'' (***Yohana 15:16;16:23***) ''Mtu haji kwa Baba,ila kwa njia ya mimi.'' ***( Yohana 14:6*****).**Hawa ni pamoja na Wayahudi,mbali na Waislamu,mbali na wakafiri,mbali na wote ambao hawajui Kristo na hawana Imani kwake kama Mkombozi.Waumini pekee ambao wamemkubali Kristo wanaweza kumkaribia Mungu kwa maombi na kumwita ''Baba,'' wengine wanaweza kubuni dua na hawahitaji kupokea majibu. Ni baada ya kupokea Kristo na kusamehewa dhambi kupitia kwa imani katika damu yake wanaweza kuwa na ''ujasiri'' wa kuingia katika patakatifu pa patakatifu kwa damu ya Yesu na kwa kuhisi kwa njia mpya ambayo ametutakasa.'' (***Waebrania 10:19,20)***.Fadhila tunazofurahia kupitia kwa Agano la Neema iliyotiwa muhuri na kuidhinishwa na damu ya Yesu,ilikuwa na ulinganifu na aina katika Israeli wa mwili na Agano la Kisheria lililotiwa muhuri na damu ya mahafali na mbuzi; kwa hiyo ilikuwa kwamba Wayahudi kama watu waliokuwa chini ya agano waliruhusiwa kumkaribia Mungu kwa maombi-japo si moja kwa moja kama sisi tulio wa Agano la Neema.

''Msipayuke-payuke kama watu wa mataifa.''Tabia ya kawaida kwa akili ya mwanadamu katika kumkaribia Muumbaji inaonekana kukosa maelezo na wanajaribu kuonyesha hayo kwa kurudia rudia.Kwa hivyo Wachina wana ''magurudumu ya maombi'' ambayo kwayo maombi marefu ambayo waumini hawawezi kukumbuka kuyarudia yanazungushwa na yeye ili kuwakilisha mapenzi yake,matakwa yake,na maombi .Kanuni hiyo pia inatumika miongoni mwa Wakatoliki ambao wanarudia ombi moja mara mia na wanaahidiwa na kuhani wao ujira fulani wa kipekee kwa ''kutamka'' maombi haya mara nyingi-kwa kukosa kufanya hivyo kutasababisha mtu ateseke siku nyingi akiwa toharani. Ushawishi kama huo pia unaonekana kufanya kazi kwa Waprotestani japo si sana,na mara nyingi unaongoza kwa maombi marefu na maagizo yasiyofaa ya kina kwa Mwenyezi.Bwana anawahitaji wafuasi wake kuomba kwa hekima na kugundua kwamba wanamkaribia Mungu mwenye hekima na akili ambaye anajua,zaidi ya vile tunavyojua,yale yote tunayohitaji na yuko tayari kutupatia kuliko vile wazazi wetu wa dunia wanaweza kupatia zawadi watoto wao.Kwa hivyo kuyarudia maombi yetu siyo kwamba ni bure kwa sababu haitatusaidia,lakini inaonyesha kiwango cha chini cha ustawi wa kiroho,dhana yasiyo mazuri ya kuheshimu Mungu,na uhusiano duni na Mungu.Mkristo hapaswi kuyarudia maombi mengine yasiodhahiri wala hapaswi kuweka kila masuala ya ulimwengu na masuala ya Kanisa,akimwambia Mungu kuhusu masuala hayo na jinsi anafaa kuyaratibisha.Tumesikia maombi ya umma ambao yaliashiria kwamba muumini alikuwa na hekima nyingi au zaidi ya Mwenyezi Mungu;kwa sababu kwa hekima yake anajaribu kumwambia Mungu Mwenyezi namna,wakati,na wapi na kile ambacho kinatakikana kifanywe kwa ulimwengu ,na nyumbani kwao na hata ng'ambo-na wangapi wanapaswa kubadilika katika mkutano ambao alikuwa akiombea na jinsi wakafiri walioko ulimwenguni kote wanapaswa kufanyiwa.

Haya yote yaonyesha kosa kubwa sana.Hakuna mtu ye yote anastahili kwa hali ya moyo wake kumkaribia Mungu katika maombi ambaye hajajifunza udhaifu na ukosefu wa hekima,na kujifunza pia maarifa ya Bwana yasiyo na kipimo na hekima na nguvu na upendo.Mkristo ambaye amekuwa na maarifa na uzoefu katika njia ya mbinguni atajazwa na utambuzi wa ujinga wake na udhaifu kiasi cha kwamba atamwendea Bwana akiomba,Bwana tufundishe mapenzi yako,nionyeshe njia yako na mpango wa wokovu kwa Wakristo na wakafiri,na nionyeshe jinsi naweza kuwa mtendakazi na wewe kwa ukamilishaji wa makusudi makuu na ya ajabu na mema.Hakika ni kwamba wakati uzoefu wa Mkristo unapokua anaweza kufikia zaidi sana kwa hali ya moyo ambapo maombi yake kwa Mungu yatakuwa hasa kushukuru kwa rehema na fadhili

ambazo amezipokea,akionyesha ujasiri katika radhi na uwezo wa kuzitimiza ahadi zote za Neno lake,za kiroho na zisizodumu na kuomba tu kwamba mapenzi ya Mungu yafanyike.

"Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba.'' Maombi ya Mkristo siyo ya kusudi la kutoa maelezo kwa Mungu,ama siyo ya kumwarifu Mungu masuala ambayo anaweza kuyasahau au kuyapuuzia;lakini kwa njia nyingine Mkristo anaamuriwa kuomba na anatakikana kuomba,kwa sababu maombi yanamsaidia yeye mwenyewe;Mungu anazuia mibaraka yake mingi hadi tumkaribie katika maombi,ili kwamba tupate kugundua kwamba twahitaji msaada wake na kumtegemea.Maombi basi siyo ya kumshawishi Mungu atupatie vitu ambavyo amevizuia ,lakini ni kupata yale ambayo anahitaji tuwe nayo na ameahidi kutupatia,na yuko tayari kutoa kuliko kuzuia.Na ni utaratibu wa kitakatifu na hekima ilioje:ni watu wa ngapi wa Mungu wamegundua faida kubwa kutoka kwa utaratibu huu kwamba lazima tuombe ili tupewe,tutafute ili tupate,lazima ''mbisheni nanyi mtafunguliwa.'' Kwa hivyo,pamoja na neema uliyoomba na kupokea,umuhimu wa maombi ni kutuleta karibu katika kushirikiana na Bwana-katika kufurahia mmoja ya fadhila na baraka kubwa.

## "BASI NINYI SALINI HIVI."

" Baba yetu uliye mbinguni,Jina lako litukuzwe.'' Kumtaja Mungu kama *Baba wetu*,kama vile tulivyoona hapo awali,haimaanishi kwamba Mungu ni baba ya wanadamu wote;kwa sababu twakumbuka kwamba Mwalimu wetu mkuu aliwaambia wengine, ''Ninyi ni wa baba yenu,ibilisi.'' Na Mtume pia alisema kwamba tulikuwa ''watoto wa uharibifu'' kama vile wengine bado walivyo. Tumekwisha ''kuyakimbia machafu yaliyo duniani,'' naye alituokoa katika nguvu za giza,akatuhamisha na kutuingiza katika Ufalme wa Mwana wa pendo lake-kutoka kwa wale watoto wa uharibifu na kutuingiza kwa familia ya Mungu; ili kwamba,sasa,kama wana wa Mungu,na wote wanaoamini katika Yesu waweze kuomba, *''Baba yetu* uliye mbinguni.'' Sehemu hii ya maombi inataja heshima,na kutambua ukuu wa Mungu,na inaonyesha unyenyekevu na udogo wetu.Inaonyesha kwamba muumini anaheshimu Mungu na hawezi kuongea naye kwa mambo yasiyofaa:hata jina la Mungu ni la kuheshimu kama takatifu na muumini wa kweli.

" Ufalme wako uje:Mapenzi yako yatimizwe,hata hapa duniani kama huko mbinguni.'' Ombi hili si la asili ya kulazimisha,ama maelezo ya kukosa subira.Bali ni la kukiri kwa muumini kwa mba ana imani katika ahadi takatifu kwamba Ufalme wa Mbinguni utasimamishwa duniani katika wakati Mungu alikusudia.Ni kukiri kwamba muumini sio kwamba ameamini tu katika ahadi za Mungu pekee lakini kwamba ana huruma na ufalme na anatamani Ufalme huo wa Bwana-yaani anatarajia Ufalme.Basi ina maana kwamba hana huruma na dhambi,na hata falme za ulimwengu huu na mpangilio wa sasa na utaratibu wake wa kijamii,kifedha,kisiasa na kidini.Ni kukubali,zaidi ya yote,kwamba muumini anatamani hali ambayo dhambi haitakuwepo-hali ambapo mapenzi ya Mungu yatafanyika duniani kama vile mbinguni.Basi ina maana kwamba hana amani na dhambi ila ana amani na haki,ukweli,na wema.Ni kukubali,hata hivyo kwamba mapenzi ya Mungu hayafanyiki duniani,kwa sababu Ufalme wake haujaja duniani bado;kwa sababu wakati ufalme wake utakuja,wakati Kristo,aliyechaguliwa kuwa Mfalme,atachukua nguvu na kutawala,matokeo ya haraka ni kama vile imeonyeshwa katika Maandiko kwamba Shetani atafungwa,maovu kwa jumla yatazuiliwa,na kwa njia nyingine maarifa,amani na baraka zitajaza dunia mzima. (***Ufunuo 20:1-3;21:1-5;22:1-6***).Hakuna vile utamwambia Bwana kinachotakikana,namna na wakati Ufalme unafaa kusimamishwa:muumini aliyeelekezwa vyema anapaswa kujua kwamba yule aliyeumba kila kitu ana uwezo kabisa kutawala na kuongoza na

kumiliki kila kitu,na kwamba yeye ndiye ‘’ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake.’’ Muumini anatakikana kuingia katika Neno takatifu kwa maagizo na atazidi kuyapokea maagizo yake akiendelea kuheshimu makusudi takatifu::katika dua hii yeye anaonyesha tu makubaliano yake yakutosha kwa utaratibu mtakatifu na anafurahia kwayo.

" Utupe leo riziki yetu.’’ Maneno haya ya Mathayo yanatofautiana kidogo na yale ya Luka.Yakifasiriwa kwa kawaida basi maelezo ya Luka ni kama haya, ‘’tupe riziki yetu kila siku,’’ Mathayo anasema ‘’leo hii,’’ wakati Luka anasema ‘’kila siku.’’ Hata hivyo,wazo bado ni moja.Hili si pendekezo kwa Mungu la kupata maridhawa na vitu vingi vilivyotunzwa kwa siku nyingi;na hata siyo ombi la kupata vitu vya kifahari;lakini ni kuuliza Bwana atupatie vitu ambavyo tunavihitaji kila siku.Kuridhika ndiyo nguvu ya sala.Ye yote aombaye Bwana kwa njia hiyo na kutoka kwa moyo wake,hakika atakuwa mtu wa shukrani na ataridhika mno.Na sala hii ni pana kama ahadi takatifu ambayo vitu vya dunia haviwezi kutoa. ‘’Chakula chake na maji yake hayatakoma,’’ kauli hiyo haitaacha nafasi ya kuomba vitu vya kifahari.Zaidi ya hayo,wakati sala hii ndiyo ombi pekee ya tabia ya kidunia,ambayo inabeba masuala na mahitaji ya kidunia,pia inaweza kueleweka kwamba inahusiana na vitu vya kiroho;na tunaamini inatumika na wana wa Mungu wote kulingana na vile wanavyokua kwa neema na katika maarifa na kiroho.Aliye na mawazo ya kiroho atakuwa anaomba chakula cha kiroho,mahitaji ya kiroho siku baada ya siku na atazidi kugundua kwamba kama vile Baba wa Mbinguni anavyovika majani ya kondeni na kuwalisha ndege wa angani,zaidi sana,atakujazi na maslahi ya kawaida yasiyodumu kwa wale wote wanaotafuta kwanza Ufalme wa Mbinguni na haki yake,-haki yenye atatekeleza.

"Utusamehe deni zetu,kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.’’ Wazo gani hilo! Nani anaweza kuomba ‘*’kwa jinsi hii’’* na bado yuko chini ya utawala wa mapepo wabaya-akiwa amejazwa na uovu,hasira,wivu,chuki,ugomvi,kutosameheana,bila shukrani,masingizio,uzushi? Kazi hizi zote za mwili na shetani zinatokana kwa hali ya uovu-hakuna mojawapo ya kazi hizo ambazo zinatokana na upendo wa kweli,kama vile Mungu alivyoingiza na Roho wake kutia msukumo.Asili ya kanuni ya Mkristo ni upendo,huruma,msamaha wa makosa ya wengine,hata tukigundua kwamba tuna makosa na Mungu ametusamehe kwa rehema yake kwa ajili ya Kristo.Bwana wetu anasisitiza umuhimu wa kuwa na roho ya msamaha kabla hatujakuwa wana wa Baba aliye Mbinguni.akisema sehemu fulani, ‘’Kwa kuwa hukumu ile mhukumuyo,ndiyo mtakayohukumuyo;’’ na kipimo kile mpimiacho,ndicho mtakachopimiwa. (***Mathayo 7:2***).Twakumbuka kwamba alitoa mfano akieleza mada iliyoonyesha mwanafunzi aliyesamehewa kama mtumishi aliyewiwa talanta kumi,ambaye alihurumiwa deni na hakumkazia tena;lakini wakati huyo mtumwa alipojazwa na roho tofauti kiasi kwamba akapata mjoli wake aliyemwia dinari yake na kumtendea vibaya bila huruma,basi huruma ya Bwana na ukarimu wake uliondolewa kwake.-Tazama ***Mathayo 18:23-35***.

Wacha kila Mkristo anapokaribia kiti cha rehema cha mbinguni,aombe kila siku kwa moyo wake,ikiwa amemsamehe wadeni wake,akihitaji kwamba Mungu atamsamehe bure kwa ajili ya Kristo.Hiyo haimanishi kuacha deni za kifedha na kuharibu vitabu vyetu vya benki,ila tu kwa mdeni ambaye ana moyo wa kulipa lakini ameshindwa kulipa,twapaswa kuwa na huruma na subira,tukitarajia huruma kutoka kwa Bwana wetu.Matumizi yake ya pekee ni wajibu wa kimaadili,kuhalifu na kuwiwa na deni.Na hili haimanishi kwamba tusijitahadhari kwa wanaotukosea-kwamba tusikose kugundua makosa.Ni kweli kwamba tusiwe wepesi wa kuona kosa,tunapaswa kutokasirika haraka.Tusiwe wepesi wa kuona makosa isipokuwa kosa *limefanywa kimakusudi.*Kwa hivyo,hata kama hatuwezi kusamehe hadi msamaha uitishwe,kulingana na mfumo wa kiungu wa mada hii,bado twapaswa kuwa na mtazamo wa kusamehe kila mara.hiyo ni kusema ya kwamba kuwa na hisia za kulipiza kisasi na uovu,hatupaswi kuwa na hisia mbaya ila tu ya upendo na huruma,na hamu ya kusamehe makosa ambayo tumetendewa,kwa haraka iwezekanavyo,na kuwa na shauku ya kufanya upatanisho kwa

njia ya ustaarabu na rahisi kwa mkosaji huyo,na tunapaswa kuwa makini kugundua na kuwa wepesi kurekebisha hatua yo yote mbaya na makosa kwa upande wetu.

Na ‘’Usitutie majaribuni lakini utuokoe kwa yule mwovu.’’ Wazo hili kidogo linavurugika;kwa sababu sote twajua kwamba ‘’ Mungu hamjaribu mtu ye yote.’’ Kueleza zaidi sentensi hii ili kwamba tupate kile tunachoamini kuwa tafsiri yake ya kawaida na kuongeza katika mabano maneno yakupendekeza ili kulifanya wazi dhana ya wazo kamili ya Bwana hapa,kama yalivyoeleweka na wale waliomsikia,fungu hili basi linasomeka hivi: ‘’Na usitulete katika majaribu (tu) lakini (pia) tuokoe kwa mwovu.’’ Ni sehemu ya mpangilio takatifu kwamba tuletwe ama turuhusiwe kupitia kwa majaribu na hukumu.Hatuwezi kuasi dhidi ya hekima takatifu inayopatikana katika suala hili,lakini kwa kinyume twakubali na kugundua kwamba majaribu ni muhimu kwa maendeleo yetu ya kiroho.Kwa hivyo,badala ya kuomba ili tusitiwe majaribuni,maombi yetu yanafaa kuwa kwamba Bwana wetu katika majaliwa yake akituleta katika mahali pa majaribu,atakuwa nasi wakati wa majaribu,na kufanya neema yake yatoshe,na asituache tujaribiwe zaidi ya uwezo wetu,na katika majaribu,atupatie njia ya kuepukana nayo-akituokoa kwa mwovu Shetani.

"Kwa kuwa ufalme ni wako,na nguvu na utukufu,hata milele,Amina. ‘’Maneno haya hata kama yanapatikana katika toleo letu la kawaida na katika muswada wa Kiyunani,hayapatikani katika Muswada wa awali ya Kiyunani., wa Kisinai na wa Vatikani.Haya yanaonekana kuwa maneno ya mwanadamu yaliyoongezwa kwa maneno ya Bwana wetu.Kulingana na vile dunia ilivyo,maneno haya hayajakuwa kweli katika awamu yote ya Injili;mamlaka ya dunia hayajakuwa ya Bwana;nguvu iliyoko duniani haijakuwa ya Bwana;na utukufu wa dunia haujakuwa wa Bwana.Kinyume ni kwamba mamlaka yamekuwa ya Shetani ‘’mfalme wa ulimwengu’’ na ametenda kazi wa wana wa uharibifu,na amepofusha akili zao wasiwazukie nuru ya injili.Na falme na nguvu za ulimwengu zimekuwa za Shetani,na watu wa Mungu wanaungojea Ufalme wa Mungu unaokuja,kama ilivyoonyeshwa katika ***mstari wa kumi***, anarudi kupindua falme za ulimwengu huu na kusimamisha Ufalme wa haki:kufunga Shetani na kuharibu kazi za mwili na za Shetani.